الزَّكَاةُ وَشُرُوطُهَا

KUCHINJA NA MASHARTI YAKE

Mwandishi:

Abu Halima Arafaat

(Allaah amsamehe yeye na wazazi wake)

UTANGULIZI WA MWANDISHI

Kila sifa njema anastahiki Allaah, na swala na salamu zimshukie Nabii wetu Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba wake.

Baada ya hayo:

Tumetangulia kutaja hukumu mbalimbali kuhusiana na mnyama anayefaa kuchinjwa katika Udh-hiya, katika Makala yetu iliyopita, baadae tukafuatishia Makala nyingine kuelezea **Hadithi dhaifu zinazofungamana na Udh-hiya**. Ni matarajio yangu kwamba tumenufaika na yale tuliyoyaona na kuyasoma ndani ya Makala hizo.

Kama inavyofahamika kwamba kuchinja ni Ibada, kwa maana hakuna anaestahiki kufanyiwa Ibada hiyo asiyekuwa Allaah; kama vile Mashetani, Mizimu n.k, basi tujue pia kwamba Ibada yoyote haitasihi mpaka kwa Ikhlaas na kumuiga Mtume ﷺ.

Na wakati ilipokuwa kuchinja mnyama kwa ajili ya Udh-hiya ni Ibada kubwa iliyo himizwa na sheria yetu tukufu, basi lazima ifanyike kwa kukamilika masharti yaliyowekwa kisheria hiyo, kinyume chake utahesabika umefanya upuuzi na hatimae kukosa ujira mbele ya Allaah ‘Azza Wajalla.

Kwa ajili hiyo nimeona (kwa taufiq ya Allaah) nikamilishe maudhui hii, kwa kuzungumzia suala la kuchinja na masharti yake, kwa sababu huenda mtu akamiliki mnyama ambaye ametimiza vigezo, lakini akawa hajui masharti ya kuchinja wala adabu zake, ikawa Makala hii (kwa rehma za Allaah) ni sababu ya kufahamu au kudiriki yule aliyesahau.

Namuomba Allaah atuonyeshe haki na aturuzuku kuifuata. Na atuonyeshe batili na aturuzuku kuiacha.

Wabillaahi Ttaufiiq.

بسم الله الرحمن الرحيم

Maana ya Dhabhu ni: kumwaga damu ya mnyama wa nchi kavu aliye halali, kwa kumchinja, (au kufanya) Nahru au kumjeruhi sehemu yoyote ya mwili wake.

Nahru ni: kumtoboa ngamia chini ya shingo (kitobwe) chake, na wakati huo atazingatiwa kisheria kuwa amechinjwa .

Ama kujeruhi: ni kwa mnyama yoyote ambaye haiwezekani kumchinja kwa njia ya kawaida, sawa awe ni ngamia, ng'ombe nyati, n.k.

Mnyama huyo ili awe ni halali kuliwa lazima yapatikane masharti yafuatayo kwa mchinjaji:

1. Awe ni miongoni mwa wenye uwezo wa kukusudia kuchinja, kama vile kuweza kupambanua (linalofaa na lisilofaa), kuwa na akili timamu, n.k, kwa hiyo haitofaa kwa mtoto mdogo kuchinja, au mzee sana asiyewaza kupambanua, kadhalika mwenda wazimu na mlevi.
2. Mchinjaji awe ni muislamu au Ahlul kitaab (anajinasibisha na Dini ya Uyahudi au Unaswara)[1], ama muislamu itajuzu hata kama ni faasiki (muovu), mtu anayefanya bidaa ambayo haimtoi katika uislamu, au mtoto mdogo mwenye kupambanua, au mwanamke.

Amesema Ibnul Mundir رَحِمَهُ اللهُ:

«وَأَجْمَعُواْ عَلَى إِبَاحَةِ ذَبِيْحَةِ الصَّبِيِّ وَالْمَرْأَةِ إِذَا أَطَاقَا الذَّبْحَ، وَأَتَيَا عَلَى مَا يَجِبُ أَنْ يُؤْتَى عَلَيْهِ»

"Wamekubaliana juu ya uhalali wa mnyama aliyechinjwa na mtoto mdogo au mwanamke endapo wataweza kuchinja, na wakafanya yale yanayopasa"[2].

[1]- Lakini akiwa atachinja kwa kulitaja jina la Allaah juu yake.
[2]- Tazama kitabu: [Al-ijmaa] (Uk. 75).

Amesema Ibn Qudama رَحِمَهُ اللهُ wakati aliponukuu maneno haya katika kitabu chake na kutaja hadithi ya mjakazi wa Ka’b Ibn Malik رَضِيَ اللهُ عَنْهُ ambaye alichinja mbuzi kwa jiwe lenye makali na Mtume ﷺ akalikubali jambo hilo:

«وَفِي هَذَا الْحَدِيثِ فَوَائِدُ سَبْعٌ: أَحَدُهَا، إبَاحَةُ ذَبِيحَةِ الْمَرْأَةِ»

“Kuna katika hadithi hii kuna faida saba: moja yao: uhalali wa kichinjwa cha mwanamke”(3).(4)

Amesema Ibn Hazmi رَحِمَهُ اللهُ:

«وَلَا أَعْلَمُ خِلَافًا فِيْ أَكْلِ مَا ذَبَحَتِ الْمَرْأَةُ الْمُسْلِمَةُ الْعَاقِلَةُ الْبَالِغَةُ عَلَى الشُّرُوْطِ الَّتِيْ ذَكَرْنَا فِيْ الرَّجُلِ»

“Wala sijui khilafu yoyote ya uhalali kula mnyama aliyechinjwa na mwanamke, muislamu, mwenye akili, baleghe, (akichinja) juu ya masharti ambayo tumeyataja kwa mwanamme”(5).

Amesema Imam Nnawawi رَحِمَهُ اللهُ:

«وَيَجُوزُ أَنْ يُوَكِّلَ كِتَابِيًّا وَامْرَأَةً وَصَبِيًّا .... وَفِي كَرَاهَةِ تَوْكِيلِ الْمَرْأَةِ الْحَائِضِ وَجْهَانِ (أَصَحُّهُمَا) لَا يُكْرَهُ لِأَنَّهُ لَمْ يَصِحَّ فِيهِ نَهْيٌ»

“Inafaa kumuweka Wakala (wa kuchinja) Ahlul kitaab (Myahudi au Mnaswara), Mwanamke na Mtoto mdogo … na kuna kauli mbili kuhusu karaha ya (kufaa) kumuwakilisha mwanamke mwenye hedhi, lakini iliyo sahihi zaidi si karaha, kwa sababu hakuna katika hilo katazo lolote”(6).

3- Tazama kitabu: [Al-Mughni] (Jz. 9, Uk. 402).

4- Tafauti na Fat-wa iliyoitolewa mwanzoni mwa miaka ya 2000m nikiwa Wete Pemba na kijana mmoja akijulikana kama Sheikh Sharifu, kwamba: [Mwanamke hafai kuchinja kwa sababu ana huruma sana]. Kauli yake hiyo ni kinyume na maelekezo ya Dini kama tulivyoona.

5- Tazama: [Maraatibul ijmaa] (Uk. 147).

6- Tazama kitabu: [Al-Majmuu’] (Jz. 8, Uk. 405).

Bali huo ndio msimamo wa Jumhuri (maulamaa walio wengi) kama alivyosema Imam Shaukani رَحِمَهُ اللهُ alipokuwa anafafanua maneno ya Mtume ﷺ alipomuamrisha Ka'b رَضِيَ اللهُ عَنْهُ kula myama yule aliyechinjwa na Mjakazi, akasema:

«فِيهِ دَلِيلٌ عَلَى أَنَّهَا تَحِلُّ ذَبِيحَةُ الْمَرْأَةِ، وَإِلَيْهِ ذَهَبَ الْجُمْهُورُ»

"Katika hadithi hii kuna ushahidi juu ya kwamba ni halali (kula) mnyama aliyechinjwa na mwanamke, na huo ndiyo msimamo wa Jumhuri (maulamaa wengi)"[7].

Na Imam Bukhari رَحِمَهُ اللهُ ameweka mlango katika sahihi yake unaosema:

«بَابُ ذَبِيحَةِ الْأَمَةِ وَالْمَرْأَةِ»

"Mlango wa kichinjwa cha Mjakazi na Mwanamke".

Amesema Ibn Hajar رَحِمَهُ اللهُ:

«كَأَنَّهُ يُشِيرُ إِلَى الرَّدِّ عَلَى مَنْ مَنَعَ ذَلِكَ»

"Kana kwamba yeye (Bukhari) anaashiria kwenye kumkosoa yule aliyekataza hilo"[8].

Kadhalika ni halali kula mnyama aliyechinjwa na Ahlul kitaab hata kama wazazi wa huyo aliyechinja si katika Ahlul kitaab. Ama asiyekuwa katika Ahlul kitaab si halali kichinjwa chake kwa ujumla wa kauli yake Allaah:

﴿ وَطَعَامُ ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡكِتَٰبَ حِلّٞ لَّكُمۡ وَطَعَامُكُمۡ حِلّٞ لَّهُمۡۖ ﴾

"Na chakula cha waliopewa kitabu ni halali kwenu"[9].

7- Tazama kitabu: [Nailul Autwaar] (Jz. 8, Uk. 160).
8- Tazama kitabu: [Fat-hul baari] (Jz. 9, Uk. 932).
9- Surat Al-Maida/5.

Amesema Al-Khaazini رَحِمَهُ اللهُ katika tafsiri yake:

«وَأَجْمَعُواْ عَلَى تَحْرِيْمِ ذَبَائِحِ الْمَجُوْسِ وَسَائِرِ أَهْلِ الشِّرْكِ مِنْ مُشْرِكِي الْعَرَبِ وَعَبَدَةِ الْأَصْنَامِ وَمَنْ لَا كِتَابَ لَهُ»

"(Waislamu wote) wamekubaliana juu ya uharamu wa vichinjwa vya majusi (waabudia moto) na baki ya washrikina, katika washirikina wa kiarabu, waabudia masanamu na yule asiye na kitabu (mpagani)"[10].

3. Awe amekusudia kuchinja, lau kama alimchinja mnyama bila kukusudia ima kwa kujihami ili mnyama huyo asimuumize, au alikusudia kukata kitu kingine lakini tahamaki akamchinja mnyama, basi si halali mnyama huyo kuliwa, kwa sababu ya kauli ya Allaah:

﴿إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ﴾

"Ila mkidiriki kumchinja"

Allaah ameegemeza kitendo cha kuchinja kwa wale anao wazungumzisha, kwa hiyo mwenye kufanya kitendo hicho atahitajia Nia kwa sababu kila amali inahitaji Nia:

«إِنَّمَا الأَعْمَالُ بِالنِّيَّاتِ، وَإِنَّمَا لِكُلِّ امْرِئٍ مَا نَوَى»

"Hakika amali zote zinahitaji nia, na hakika kila mtu atalipwa vile alivyonuwia"[11].

4. Asichinje kwa kumkusudia asiyekuwa Allaah[12], kama kujikurubisha kwa sanamu, mzimu, kaburi, au kuchinja kwa kukumsudia mfalme, rais au mheshimiwa fulani, na akichinja kwa sababu hizo mnyama huyo si halali kuliwa hata akitamka Bismillaahi, kwa hadithi:

10- Tafsiirul Khaazin (Jz. 2, Uk. 13).
11- Bukhari (1). Muslim (155).
12- Kama vile Shetani, Mzimu n.k.

«وَلَعَنَ اللهُ مَنْ ذَبَحَ لِغَيْرِ اللهِ»

“Allaah amlaani aliyechinja kwa kumkusudia asiyekuwa Allaah”[13].

5. Asitaje lisilo kuwa jina Allaah, kama vile jina la Nabii (Bismi Nnabiy), Malaika: (Bisimi Jibril), au mzimu Fulani n.k.

Allaah amesema:

﴿حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ ٱلْمَيْتَةُ وَٱلدَّمُ وَلَحْمُ ٱلْخِنزِيرِ وَمَآ أُهِلَّ لِغَيْرِ ٱللَّهِ بِهِۦ﴾

“Mmeharimishiwa nyamafu (mzoga), damu, nyama ya nguruwe na mnyama aliye chinjwa kwa (kutajwa) lisilo kuwa jina la Allaah”[14].

Amesema Ibn Kathiir رَحِمَهُ اللهُ katika kuitafsiri aya hii:

«مَا ذُبِحَ فَذُكِرَ عَلَيْهِ اسْمُ غَيْرِ اللَّهِ، فَهُوَ حَرَامٌ؛ لِأَنَّ اللَّهَ أَوْجَبَ أَنْ تُذْبَحَ مَخْلُوقَاتُهُ عَلَى اسْمِهِ الْعَظِيمِ، فَمَتَى عُدِلَ بِهَا عَنْ ذَلِكَ وَذُكِرَ عَلَيْهَا اسْمُ غَيْرِهِ مِنْ صَنَمٍ أَوْ طَاغُوتٍ أَوْ وَثَنٍ أَوْ غَيْرِ ذَلِكَ، مِنْ سَائِرِ الْمَخْلُوقَاتِ، فَإِنَّهَا حَرَامٌ بِالْإِجْمَاعِ»

“Mnyama yoyote aliye chinjwa halafu likatajwa juu yake lisiluwa jina la Allaah, basi (mnyama) huyo ni haramu, kwa sababu Allaah amewajibisha wachinjwe viumbe (wanyama) wake juu ya (kutajwa) jina lake tukufu, basi wakati wowote akiepushwa (mnyama) huyo na hilo (jina la Allaah) kisha likatajwa juu yake jina la mwingine asiyekuwa yeye Allaah, (jina la) sanamu, shetani, mzimu, au viumbe wengine, basi mnyama huyo ni haramu (kuliwa) kwa makubaliano ya maulamaa (wote)”[15].

6. Ataje jina la Allaah juu yake, kwa ajili ya kauli yake Allaah:

﴿فَكُلُوا۟ مِمَّا ذُكِرَ ٱسْمُ ٱللَّهِ عَلَيْهِ إِن كُنتُم بِـَٔايَـٰتِهِۦ مُؤْمِنِينَ﴾

13- Muslim (43).
14- Suratul Maida/3.
15- Tafsiri ibn kathiir (Jz.3, Uk. 17).

"Basi kuleni katika walio somewa jina la Allaah juu yake. Mkiwa nyinyi mnaziamini Aya zake"[16].

Na pia amesema:

﴿وَلَا تَأۡكُلُواْ مِمَّا لَمۡ يُذۡكَرِ ٱسۡمُ ٱللَّهِ عَلَيۡهِ وَإِنَّهُۥ لَفِسۡقٞۗ﴾

"Wala msile katika wale wasio somewa jina la Allaah juu yake. Kwani huo ni upotofu"[17].

Na Mtume ﷺ amesema:

«مَا أَنْهَرَ الدَّمَ، وَذُكِرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ فَكُلُوهُ»

"Kitu chochote ambacho kimemwaga damu[18] na likatajwa juu yake (mnyama huyo) jina la Allaah, basi kuleni"[19].

a. Sharti ni kwamba atamke jina la Allaah wakati wa kupatikana kitendo hicho cha kuchinja, wala pasiwepo baina yake kipambanuzi chochote, (mfano) akasema: Bismillaahi, kisha akaenda kunywa maji, halafu akarejea na kumchinja mnyama huyo haitafaa, kwa sababu hiyo ni dhikri maalumu ambayo sharti lake ni kuwa itamkwe wakati wa tukio, na kama ni kipambanuzi kidogo kiasi cha kumlaza mnyama vizuri na kumchinja hapana tatizo.
b. Atamke jina la Allaah kwa mnyama aliyemkusudia kumchinja, akitamka hali ya kuwa amemshika mbuzi kisha akabadilisha na kumchukua mwingine basi atamke upya.
c. Inatakiwa atamke jina la Allaah kwa kusema: (Bismillaahi).

16- Suratul An-aam/118.
17- Suratul An-aam/221.
18- Anakusudia kitu chochote kinachoweza kuchinja na kikamwaga damu, sawa ni Kisu, kigae nk. au jiwe lenye makali n.k basi inafaa kukitumia katika kuchinja.
19- Bukhari (2488) na Muslim (24).

d. Haifai mtu kuacha kwa makusudi kutamka jina la Allaah (Bismillaahi), kwa sababu Mtume ﷺ ameweka sharti kwa mnyama ili awe ni halali kuliwa, basi kitumike kitu chenye kumwaga damu na litajwe juu yake jina la Allaah, mpaka baadhi ya Maulamaa wanaona kwamba kutamka Bismillaahi wakati wa kuchinja ni sharti, lau mtu aliacha kwa ujinga au kusahau basi mnyama huyo si halali kuliwa (ni mzoga). Lakini wengine wanaona kuwa ni sunna, endapo mtu ameacha kutamka bado mnyama huyo atakuwa halali, kwa hiyo muislamu ajitahidi kutamka wala asiache.

e. Asiikusudie Bismillaahi kwa moyo bali aitamke kwa ulimi, na akiwa hawezi kama vile bubu basi atatoa ishara pekee.

7. Achinje kwa kitu chenye makali (chenye kukoa) lakini si kucha wala jino, kwa sababu kucha ni mfupa, na haifai kuchinja kwa kutumia mfupa wa aina yoyote, vile vile kucha, kwa sababu ni kisu cha Wahabeshi, na baadhi ya Maulamaa wanasema sababu ya kukatazwa kwake ni:.

   a) Itapelekea watu kufuga kucha kwa ajili ya kuzitumia katika kuchinja, na kama inavyojulikana katika sheria ya kiislamu kwamba haifai mtu kufuga kucha zake kwa kuzirefusha.

   b) Kuchinja kwa kutumia kucha ni kujishabihisha na ndege au wanyama wakali wenye kushambulia, ambao sisi tumefadhilishwa juu yao na tumekatazwa kujifananisha nao.

8. Kuhakikisha kwamba anamwaga damu, na hilo lina hali mbili:

   a) Endapo mnyama imeshindikana kumkamata ima kwa kuwa amekimbia au ametumbukia kisimani, kiasi ambacho haiwezekani kumpata na kumchinja kwa njia ya kawaida, basi katika hali hii atapigwa kwa kuchomwa sehemu yoyote ya mwili wake mpaka afe, na iliyo bora itumike zana ambayo itaweza kumtoboa na kumuua kwa haraka, wala lisitumike mfano wa rungu au fimbo n.k, kwa sababu haviwezi kumtoboa na kumwaga damu.

b) Ama akiwa ni mnyama ambaye anaweza kudirikiwa basi ni sharti achinjwe katika shingo yake, kwa kukata mshipa mkubwa wa pumzi, chakula na kinywaji, na mishipa miwili minene iliyozunguka mshipa wa pumzi na mshipa wa chakula na kinywaji.

9. Awe mchinjaji ameruhusiwa kisheria, na kama hajapewa ruhusa kisheria basi ana hali mbili:

a) Ni kuwa amezuiwa kuchinja kwa ajili ya haki ya Allaah, mfano kuwinda kwa mtu aliyehirimia Hija au Umra, mtu huyo akiwinda mnyama, akamchinja hali ya kuwa amehirimia basi mnyama huyo ni haramu kuliwa, kwa kauli ya Allaah:

﴿وَحُرِّمَ عَلَيْكُمْ صَيْدُ ٱلْبَرِّ مَا دُمْتُمْ حُرُمًا﴾

"Na mmeharimishiwa kuwinda wanyama wa bara muda wa kuwa mmehirimia"[20].

b) Au amezuiwa kwa ajili ya haki ya mwanadamu, mfano kumchinja mnyama ambaye hammiliki wala hajapewa ruhusa na mwenyewe, au mnyama wa wizi n.k. ni haramu kula mnyama huyo kwa mchinjaji na kila aliyejuwa kuwa mnyama huyo si halali.

****

[20]- Suratul Maida/96.

Adabu za kuchinja:

Kama ilivyokuwa kuchinja kuna masharti ambayo huzingatiwa pia kuna adabu ambazo inapasa kuzijua, miongoni mwa hizo:

1. Kumuelekeza mnyama upande wa kibla.
2. Kumtendea wema, kwa kutumia kifaa chenye makali.
3. Kupitisha mkono wake kwa nguvu shingoni kwa mnyama.
4. Ngamia huchinjwa hali ya kuwa amesimama kwa miguu mitatu na huku mguu wake wa kushoto ukiwa umenyanyuliwa juu umefungwa, na anachinjwa kwa kutobolewa chini ya kitobwe cha shingo yake.
5. Asiyekuwa ngamia huchinjwa hali ya kuwa amelazwa kwa ubavu wake wa kushoto na huku mchinjaji akiweka mguu wake juu ya shingo yake, na anayetumia mkono wa kushoto basi atamlaza kwa ubavu wa kulia, na ashike kichwa chake na kukinyanyua kidogo ili aone vizuri mahala pa kuchinja, wala asimzuie mnyama mikono na miguu yake wakati wa kumchinja, lakini ikipelekea kufanya hivyo basi iwe kwa upole ili aweze kujitikisa na kutoa damu kwa wingi.
6. Kukamilisha kukata mshipa wa pumzi, mshipa unaopita chakula na kinywaji, na mishipa miwili migumu iliyo pembezoni mwake.
7. Asitoe kisu chake isipokuwa wakati wa kutaka kuchinja.
8. Kuleta takbira baada ya kutaja jina la Allaah: (Bismillaahi wallaahu akbar).
9. Kutaja jina la mwenye mnyama huyo wakati wa kuchinja Udh-hiya au ‘Aqiiqa, lakini hata kama atakusudia tu kwa moyo wake itafaa.
10. Kuomba dua baada ya kumaliza kuchinja:

«بِاسْمِ اللهِ، اللهُمَّ تَقَبَّلْ مِنْ مُحَمَّدٍ، وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَمِنْ أُمَّةِ مُحَمَّدٍ»

“Bismillaahi, ewe Allaah mkubalie Muhammad, Jamaa zake, na umati wake”[21].

[21]- Muslim (19).

Mambo ya karaha wakati wa kuchinja

1. Kuchinja kwa kutumia kifaa kisicho na makali.
2. Kumchinja mnyama mmoja hali ya kuwa mwenzie anatazama.
3. Kumfanyia mambo ya karaha kabla ya kumchinja, kama vile kumvunja kiungo chake, bali kauli sahihi ni haramu kufanya jambo hilo.
   - Kumtolea maneno yasiyofaa; kama kusema, leo ndio mwisho wako, utakoma n.k.
4. Kunoa kisu hali ya kuwa mnyama huyo anakiona.

Wallaahu A'lam.

Namuomba Allaah atupe elimu yenye manufaa, atutakabalie ibada zetu na atughufirie madhambi yetu.

Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud

Leo Al-khamis 8/Dhul-hijja/1443^{H} – 7/7/2022^{M}

Markaz sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah

Tanga Pongwe.

Simu: 0715263253